# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA KILWA

**KABRASHA LA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO KITAKACHOFANYIKA TAREHE 26 MEI, 2022 KUJADILI TAARIFA YA ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI MACHI 2022**


***Imetayarishwa na:-***
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
SLP.160
SIMU No.023-2013065
FAX No.023-201365
KILWA MASOKO

**AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO KITAKACHOFANYIKA TAREHE 26 MEI, 2022 KUJADILI TAARIFA YA ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI MACHI 2022 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI**

1. KUFUNGUA KIKAO.
2. KUTHIBITISHA AGENDA.
3. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 24 MACHI, 2022
4. YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 24 MACHI, 2022
5. TAARIFA ZA MIJI MIDOGO KILWA KIVINJE NA KILWA MASOKO
6. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2022
7. TAARIFA YA MANUNUZI KWA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DESEMBA, 2021
8. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI MACHI 2022
9. TAARIFA KUHUSU KESI ZA HALMASHAURI
10. TAARIFA YA IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA
11. TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI MACHI 2022
12. TAARIFA YA UTOAJI WA MIKOPO KWENYE VIKUNDI VYA WANAWAKE VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU
13. MAPENDEKEZO YA KUJENGA KITUO CHA AFYA KATIKA KATA YA MIGURUWE KIJIJI CHA ZINGA KIBAONI
14. MAPENDEKEZO YA KUMLIPA MWENYEKITI WA HALMASHAURI KIASI CHA TSH.230,000 KWA AJILI YA MAWASILIANO.
15. MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.
16. KUFUNGA KIKAO.

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 24 MACHI, 2022 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA.KUJADILI TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA KUISHIA TAREHE 28 FEBRUARI, 2022

**A. MAHUDHURIO YA WAJUMBE.**

| NA.JINA | WADHIFA/CHEO |
|---|---|
| 1. Mhe. Farida M. Kikoleka | Mwenyekiti na Diwani kata ya Miguruwe. |
| 2. Mhe. Francis Ndulane | Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini |
| 3. Mhe. Jafari Arobaini | Diwani kata ya kivinje. |
| 4. Mhe. Ngwinde Mketo | Diwani kata ya Kibata. |
| 5. Mhe. Haji R. Chijinga | Diwani kata ya Masoko. |
| 6. Mhe. Nasoro Kimbugu | Diwani kata ya Kandawale. |
| 7. Mhe. Rukia Jamadali | Diwani viti maalumu. |
| 8. Mhe. Nuru Likologelo | Diwani viti maalum. |

**B.WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | |
|---|---|
| Mhe. Francis Ndulane | Mbunge Jimbo la Kilwa Kaskazini |
| Mhe. Ally Kassinge | Mbunge Jimbo la Kilwa Kusini |

**C. KATIBU**

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. John Mkinga | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya |

**D. WATAALAMU.**

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Liku Dotto | Kaimu Afisa Utumishi Wilaya |
| 2. Ndg. Fadhili Izumbe | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 3. Ndg. Fauza Issa | Kaimu Afisa Mazingira(W) |
| 4. Ndg.Maulidi Kikali | TEO Kivinje |
| 5. Ndg. Mkuwili O.S | Katibu TSC Wilaya |
| 6. Ndg. Erick Nkinda | Kaimu Afisa Mipango Wilaya |
| 7. Ndg. Emanuel Kayeta | Mkaguzi wa Ndani |
| 8. Ndg. Abushiri Mbwana | Afisa Ufugaji Nyuki Wilaya |
| 9. Ndg. Ahmadi Habibu | Afisa Uvuvi Wilaya |
| 10. Ndg. Grace Mwambe | Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya |
| 11. Ndg. Ally Ligalawike | Uchaguzi Wilaya |
| 12. Ndg. Juliana Chikoti | Mratibu wa Lishe |
| 13. Ndg. Silvester Kalagila | Afisa Elimu Msingi Wilaya |
| 14. Ndg. Khajui Bofu | Kaimu Afisa Elimu Sekondari Wilaya |
| 15. Ndg. Sifaeli Mwanyehesi | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi Wilaya |
| 16. Ndg. Michael Kabanda | Afisa Mtendaji Mji Mdogo Kilwa Masoko |
| 17. Ndg. Stella Omari | Mratibu TASAF |

18. Ndg. Vicenti Muhengilolo — Kaimu Afisa Ushirika Wilaya
19. Ndg. Charity Ngenzi — Afisa Ustawi wa Jamii
20. Adv. Godfrey Jafari — Mkuu wa kitengo cha Sheria
21. Ndg.Tunu S. Mtamah — Afisa Manunuzi
22. Eng. Saidi Pongwa — Mhandisi wa Ujenzi wilaya.

**D. SEKRETARIETI**

1. Ndg. Joseph Ng'onja — Mwandishi wa Vikao
2. Ndg. Mohamedi S. Wangeleja — Mwandishi wa Vikao
3. Ndg. Julius Mayega — Mwandishi wa Vikao

**2/2022. KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alisimama na kuwakaribisha wajumbe katika kikao, aliwaeleza kuwa kikao hicho ni cha kawaida ambacho kitajadili taarifa za utekelezaji za kipindi cha mwezi Februali 2022. Alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe, aliwaeleza kuwa kikao ni cha kawaida, akawataka wajumbe pamoja na wataalamu washirikiane kujadili agenda hizo kwa ajili ya ustawi wa Halmashauri. Kikao kilifunguliwa mnamo saa 7:30 Mchana.

**3/2022.KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu aliwasilisha jumla ya Agenda saba (7) zijadiliwe katika kikao hicho ambapo wajumbe walipokea na kuridhia agenda hizo zijadiliwe katika kikao hicho.

**4/2022.KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 15 MACHI, 2022**

Muhtasari wa kikao cha kamati ya fedha uongozi na mipango kilichofanyika tarehe 15 Machi, 2022 uliwasilishwa, wajumbe waliupokea na kuupitia ukurasa kwa ukurasa hatimaye wakauthibitisha kuwa kumbukumbu halali za Halmashauri.

**5/2022.YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 15 MACHI, 2022**

Yatokanayo na kikao cha kamati ya fedha uongozi na mipango kilichofanyika tarehe 24 Machi, 2022 yaliwasilishwa, wajumbe walipokea na kuridhia baadhi ya utekelezaji wa maagizo ya kikao kilichopita ,aidha wajumbe walihitaji ufafanuzi Zaidi katika maagizo yafuatayo ifuatavyo;

5.1 **Kuhusu Madeni ya wajumbe wa Mamlaka ya Mji Mdogo Kilwa Kivinje.**

Mjumbe alihoji kama Afisa mtendaji Mkuu wa Maml
jiridhisha na madeni ya wajumbe wa mamlaka kama alivyoagizwa kwenye kikao kilichopita cha kamati ya fedha,uongozi na mipango.

Afisa mtendaji mkuu wa mamlaka alitoa ufafanuzi kuwa madeni yaliyohakikiwa ni kuanzia mwaka 2019/2020,aidha alieleza kwamba amejiridhisha na madeni yaliyowasilisha na madeni hayo aliyapitia na wajumbe wanaodai posho zao pamoja na kamati ya fedha,uongozi na mipango ya mamlaka ya mji mdogo Kilwa kivinje.
Wajumbe walipokea taarifa nakuridhia.

**5.2 Kuhusu malalamiko ya wakulima wa ufuta wa Nanjirinji kulipwa madeni yao ya mauzo ya ufuta katika msimu uliopita.**

Afisa Ushirika alitoa ufafanuzi kuwa taarifa ya mrajisi imesambazwa katika vyombo mbalimbali vya usalama na mrajisi atafika Nanjirinji kuzungumza na wakulima,aidha mrajisi ameeleza kuwa kikao cha kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango hakina mamlaka yakupata taarifa hizo.

Mheshimiwa Ngwinde alieleza kuwa kama kamati ya fedha,uongozi na mipango hakina mamlaka ya kupata taarifa ya wakulima wanaodai fedha za mauzo ya ufuta katika chama cha msingi Nanjirinji, alishauri suala hili lipelekwe katika ngazi za juu kwa ufuatiliaji Zaidi.

Mheshimiwa Arobaini aliunga mkono hoja kuwa jambo hili limekuwa na utata,na imepita karibu miezi sita tangu wakulima hawa waanze kufuatilia haki zao za wakulipwa madeni yao na chama cha msingi Nanjirinji,alishauri suala hili liende ngazi ya juu kwa ufuatiliaji Zaidi.

Mwenyekiti alieleza kuwa wakulima walikubaliana na chama cha ushirika namna yakupokea mazao yao kwenye ghala na baadaye kufanyika minada,aidha wakulima hawa leo wanataabika kudai fedha zao,aliunga mkono hoja kuwa jambo hili tulipeleke mkoani Lindi kwa ufafanuzi Zaidi.

Wajumbe waliazimia kuwa wakulima wa ufuta wa Nanjirinji wanaodai fedha zao za mauzo ya ufuta katika msimu uliopita watafuatilia Mkoani kabla ya Kikao kijacho.

**25.3. Kuhusu malipo ya posho ya wajumbe wa kamati ya kudhibiti maambukizi ya Ukimwi ambao si waheshimiwa madiwani waliojadili makisio na mpango wa bajeti 2022/23.**

Mjumbe alihoji sababu za kutolipwa posho za wajumbe ambao si madiwani wa kamati ya Kudhibiti maambukizi ya Ukimwi.

Kaimu mweka hazina atoa ufafanuzi kuwa kuwa malipo wa jumbe hao yanaandaliwa na watalipwa muda wowote kuanzia sasa.

Wajumbe waliopokea taarifa hiyo na kuazimia kuwa malipo hayo yafanyike mapema kwakuwa ni haki yao kulipwa fedha zao za posho ya kikao.

**25.4 Kuhusu mapato ya ufuta yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha 2019/2020 na 2020/2021 kuwa kuna utofauti wa mapato ya kufungia mwaka kwenye makabrasha na taarifa yakufungia mwaka iliyopo kwenye mfumo.**

Taarifa ya Mwekahazina ilionyesha kuwa taarifa zilizo fungiwa mwaka ambazo zipo kwenye mfumo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni **Tsh.1,740,372,618.93** na mwaka wa fedha wa 2020/2021 ni **1,182,417,595.94.**

Mwenyekiti alieleza kuwa suala hili liliazimiwa kwenye mkutano wa baraza kuwa wajumbe wajiridhishe na fedha iliyopo kwenye mfumo na ile iliyoletwa kwenye kikao kufungia kikao.

Kaimu Mwekahazina alieleza kuwa atafuatilia na kuleta ufafanuzi kikao kijacho.

**/2022.TAARIFA ZA MIJI MIDOGO.**

**Taarifa za miji midogo ya Kilwa masoko na Kilwa Kivinje iliwasilishwa kama ifuatavyo;**

**26.1 MAMLAKA YA MJI MDOGO KILWA MASOKO.**

Kaimu Afisa mtendaji mkuu wa mamlaka ya mji mdogo Kilwa Masoko aliwasilisha taarifa ya taarifa ya mapato na matumizi ya Mamlaka ya mji mdogo Kilwa Masoko kuishia mwezi februari 2022.Taarifa ilieleza kuwa Mwaka wa fedha **2022**. Mamlaka ya Mji Mdogo Kilwa Masoko iliweka lengo la kukusanya jumla ya **Tshs 160,000,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani.

Mapato kuanzia **mwezi Julai** hadi **february 2022** ni **Tshs 78,454,532.00**. Mapato ya Mwezi February pekee ni **Tshs 10,062,900.00 na** kufanya mapato toka **Julai hadi februari 2022** kuwa **tshs 86,237,432.00** sawa na asilimia **53.9** ya makusanyo yote ya Mamlaka ya Mji Mdogo Kilwa Masoko.

Kwa upande wamatumizi Taarifa ilieleza kuwa matumizi kuaniza mwezi **Julai hadi** February 2022 ni Tshs 27,319,500.00. Matumizi ya mwezi Febeuary 2022 pekee alikuwa Tshs 28,434,500.00 sawa na asilimia 17.77

**MAFANIKIO**

1. Vikao vya Kisheria vinafanyika
2. Vibarua wamelipwa mishahara yao mpaka mwezi february 2022
3. Wenyeviti wa Mamlaka wamelipwa posho zao za mwezi hadi february 2022

**CHANGAMOTO**

- Kucheweshwa kulipwa madeni ya Posho za wenyeviti na posho za vikao kwa wenyeviti waliomaliza mda wao.
- Wafanyabiashara wa vibanda vya stendi kutolipa madeni yao kwa wakati na baadhi ya wafanyabiashara kuamua kujenga mabanda yao ya biashara bila ya kuja ofisini kuonana na afisa Mtendaji mkuu wa Mamlaka kupata Kibali cha ujenzi pamoja na ramani.

**MIKAKATI YA KUKUSANYA MAPATO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022/2023**

- Kuoneza uubunifu wa ukusanyaji wa vyanzo vipya vya mapato.
- Kuendelea kusimamia mikakati ambayo iliyotuwezesha kuvuka lengo katika eneo la ukusanyaji wa mapato ya ndani **2021/2022**
- Kufanya ukaguzi wa kustukiza katika mageti na minada ya samaki.
- Kufanya doria za mara kwa mara Baharini na nchi kavu.
- Kuongeza idadi ya wakusanyaji ushuru kwa wakati pindi panapohitajika.
- Kukusanya ushuru kwa wafanyabiashara wanaouza samaki kwa wakongo.
- Kuendelea kuwasimamia kwa ukaribu wakusanyaji wote wa ushuru
- Watumishi wa Mamlaka wamepangiwa maeneo ya kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu vyanzo vya mapato ili kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato.
- Timu ya kufuatilia madeni ya wamilki wa mabanda ya biashara katika eneo soko la masoko kuendelea na kazi.
- Timu yakuafuatilia madeni inaendelea kufanya kazi yake ya kuongea na wamiliki wa mabanda ili wawe tayari kuwa kulipa madeni yao bila usumbufu.
- Kutoa elimu ya madhara ya ukwepaji wa kulipa ushuru waamlaka ya mji ya mji mdogo kilwa masoko,kwa kila kitongoji ambavyo vinajishughulisha n asana na uvuvi.

Wajumbe walipokea taarifa nakuridhia.

## 26.2. MAMLAKA YA MJI MDOGO KILWA KIVINJE.

Afisa mtendaji mkuu wa mamlaka aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha Julai Hadi Februari, 2022.

Taarifa Hii Imegawanyika Katika Sehemu Mbili Kama Ifuatavyo:

- **Sehemu ya kwanza ni mapato**
- **Sehemu ya pili ni Matumizi.**

### 1. MAPATO

Katika Kipindi Cha Mwaka Wa Fedha 2021/2022. Mamlaka iliweka Malengo Ya Kukusanya **Tsh.486,653,330.00** Kutoka Vyanzo Vya Mapato Ya Ndani.

Mapato Kuanzia Julai – Februari, 2021 Ni **Tshs 296,248,995.50, sawa** na Asilimia **61% ya** lengo la Makusanyo Yote. Mapato Ya mwezi Februari 2022 ni Tshs **40,425,462.08**

### 2. MATUMIZI

Taarifa Ya Matumizi Kuanzia Julai – Februari, 2022 Ni **Tshs 42,207,900.00** Sawa Na Asilimia **8.67%** Na Matumizi Mwezi Februari, Ni **Tshs 3,675,500.00**

Taarifa ya mapato na Matumizi imeambatanishwa.

- **MAFANIKIO**

1.Vikao Vya Kisheria Vinafanyika

2.Vibarua Wamelipwa Mishahara Yao Mwezi Februari, 2022.

3.Wenyeviti Wamelipwa Posho Ya Mwezi Hadi Mwezi Februari, 2022.

4. Tumepata Mizani moja ya kupimia mizigo ya samaki kutoka Halmashauri (W).mizani hiyo tumeiweka Eneo la stand ya magari kivinje

- **CHANGAMOTO**

1.Kucheleweshwa Kulipwa Madeni Ya Posho Za Madaraka Na Vikao Kwa Wenyeviti Waliomaliza Muda Wao

2.Kutokukamilika Ujenzi Wa Soko La Mnada Wa Samaki Na Choo.

3.Wafanyabiashara Wa Vibanda Vya Stendi Na Jukwaa La Maalim Seif Kutokulipa Madeni Yao Ya Pango Kwa Wakati.

**MIKAKATI YA KUKUSANYA MAPATO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2021/2022.**

1.Kuongeza Ubunifu Wa Vyanzo Vipya Vya Ukusanyaji Mapato Ndani Mamlaka .

2.Kuendelea Kusimamia Mikakati Iliyotuwezesha kuvuka Lengo Kwa Kipindi Cha Mwaka 2021/2022

4.Kufanya Ukaguzi Wa Kushitukiza Katika Mageti Yaliyopo Ndani Ya Mamlaka.

5.Kufanya Doria Za Kushitukiza Baharini Na Nchi Kavu..

6.Kuendelea Kuwasimamia Kwa Karibu Wakusanyaji Wa Ushuru Wa Mamlaka

7.Kukusanya Ushuru Kwa Wafanyabiashara Wanaouza Samaki Kwa Wakongo.

8.Watumishi wa Mamlaka ya Mji Mdogo na kata Wamepangiwa maeneo ya kusimamia na kufuatilia ushuru katika Vyanzo Vyetu vya Mapato

Wajumbe walipokea nakujadili taarifa hiyo kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Arobaini alieleza changamoto ya kutokuwepo kwa mlinzi Hospitali ya wilaya Kinyonga na uzio,aidha alieleza kuwa mali za hospitali zinaweza kuibiwa kwa kuwa hakuna usalama katika eneo lile.

Mheshimiwa Ngwinde alieleza kuwa tumeona bajeti ya maombi ya Tsh.10,000,000 kwa ajili ya uzio Hospitali ya wilaya Kinyonga,changamoto iliyopo kwa sasa ni mlinzi.

Mganga mkuu wa wilaya alieleza kuwa ni kweli hakuna walinzi na uzio katika hospitali ya Wilaya Kinyonga,aidha alieleza kuwa tumeshaomba Tsh.10,000.000 kwa ajili ya kuweka uzio,suala la mlinzi akaeleza kuwa atalifanyia kazi na kikao kijacho ataleta mrejesho.

Wajumbe waliazimia kuwa kikao kijacho tupate taarifa suala la kuajiriwa walinzi Hospitali ya Wilaya imefikia hatua gani.

**/2022.TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA KUISHIA MWEZI FEBRUARI,2022**

Mh. Mwenyekiti Mwaka wa Fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya Kilwa imekisia kukusanya jumla ya shilingi **33,934,224,000.00** kwenye vyanzo yake vya mapato ya ndani, Ruzuku ya Mishahara, Ruzuku ya matumizi mengineyo na Miradi ya maendeleo. Pia Halmashauri ilivuka na bakaa ya **Tsh.297, 948,094.21** ambazo Tsh. **55,818,226.11** ni fedha za amana, tsh. **78,772,973.83** ni fedha za mfuko wa wanawake na vijana naTsh.**163, 356,894.27** ni fedha za Halmashauri kutokana na mapato ya ndani. Pia Halmashauri imevuka na fedha Tsh. **700,405,449.78** Kwenye akaunti za shule za msingi, shule za sekondari, zahanati, vituo vya afya na hospital ikiwa ni fedha za miradi iliyoko kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na elimu pamoja na mapato ya ndani ( fungiwa) kwa mchanganuo ufuatao :

**Jedwali la mchanganuo wa bakaa za vituo vya kutolea huduma**

| KITUO | CHANZO CHA FEDHA | KIASI KILICHOBAKI | JUMLA |
|---|---|---|---|
| **Hospital ya Wilaya** | Miradi | 12,439,159.97 | **25,359,008.73** |
| | Mapato ndani fungiwa | 12,919,848.76 | |
| **Vituo vya Afya** | Miradi | 13,678,433.15 | **21,813,866.30** |
| | Mapato ndani fungiwa | 8,135,433.15 | |
| **Zahanati** | Miradi | 232,816,183.56 | **271,449,222.86** |
| | Mapato ndani fungiwa | 38,633,039.30 | |
| **Shule za Sekondari** | Miradi | 265,701,429.87 | **266,444,305.80** |
| | Mapato ndani fungiwa | 742,875.93 | |
| **Shule za Msingi** | Miradi | 123,339,046.09 | **123,339,046.09** |
| | Mapato ndani fungiwa | 0 | |
| **JUMLA KUU** | | | **708,405,449.78** |

**Jedwali la Makisio ya Mwaka Julai 2021 hadi Juni 2022**

| CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO |
|---|---|
| Mapato ya ndani | 4,003,173,500.00 |
| Mapato ya ndani fungiwa | 1,496,641,000.00 |
| Matumizi mengineyo | 672,490,000.00 |
| Ruzuku y Mishahara | 16,864,799,000.00 |
| Ruzuku ya miradi ya maendeleo | 10,826,726,500.00 |
| **JUMLA KUU** | **33,863,830,000.00** |

Pia halmashauri imepokea fedha za miradi zilizokuja Kwa maelekezo maalumu jumla ya Tsh **3,424,783,022.51** hivyo kufanya jumla ya fedha za miradi kua Na bajeti ya Tsh **14,251,509,522.51** hvyo kufanya jumla kuu ya bajeti kufikia Tsh **37,359,007,022.51**

**Jedwali la fedha zilizopokelewa Kwa maelekezo maalum Kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

| CHANZO CHA FEDHA | KIASI |
|---|---|
| Ujenzi wa vituo vya Afya hotel tatu na kipindimbi | 750,000,000.00 |
| Chanjo COVID 19 awamu ya kwanza | 33,224,000.00 |
| COVID 19 Madarasa sekondari | 1,480,000,000.00 |
| COVID 19 Madarasa shule za Msingi | 580,000,000.00 |
| CIVID 19 Nyumba ya Mtumishi | 90,000,000.00 |
| COVID 19 Jengo huduma za Dharula | 300,000,000.00 |
| COVID 19 Uhamasishaji wa chanjo | 41,651,075.51 |
| COVID 19 Uhamasishaji na Tathmini | 6,514,747.00 |

| | |
|---|---|
| COVID 19 Ajira ya muda | 5,214,400.00 |
| KOICA | 138,178,800.00 |
| **JUMLA KUU** | **3,424,783,022.51** |

**Jedwali la mchanganuo wa mapato ya ndani kwa Mwezi February, 2022**

| CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO | MAPATO HALISI | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|
| Halmashauri ya wilaya ya kilwa | 3,356,520,170.00 | 92,910,199.67 | 2.76 |
| Mapato ya ndani fungiwa | 1,496,641,000.00 | 27,137,210.00 | 1.26 |
| Mamlaka ya mji mdogo Masoko | 160,000,000.00 | 10,062,900.00 | 6.28 |
| Mamlaka ya mji mdogo Kivinje | 486,653,330.00 | 40,425,462.8 | 8.3 |
| **JUMLA KUU** | **5,499,814,500.00** | 170,535,772.47 | **3.12** |

**Jedwali la mchangunuo wa mapato kwa ujumla hadi kufikia tarehe 28 February 2022**

| CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO | MAPATO HALISI | ASILIMIA% |
|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani | 4,003,173,500.00 | 2,572,607,420.33 | 64.26 |
| Mapato ya ndani fungiwa | 1,496,641,000.00 | 943,698,887.55 | 63.05 |
| Ruzuku ya matumizi menginevyo | 742,884,000.00 | 635,749,032.76 | 85.58 |
| Ruzuku ya mishahara | 16,864,799,000.00 | 11,696,263500.00 | 66.35 |
| Ruzuku ya miradi ya maendeleo | 14,251,509,522.51 | 9,022,799,369.64 | 63.27 |
| **JUMLA KUU** | **37,359,007,022.51** | **24,871,118,210.28** | **66.56** |

**Matumizi hadi kufikia 28 February 2022 ni kama ifuatavyo kwenye jedwali hapo chini.**

| [illegible]NZO CHA [illegible]PATO | MAKISIO | BAKAA | JUMLA YA MAKISIO NA BAKAA | MATUMIZI HALISI | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|---|
| [illegible] ya [illegible] | 4,003,173,500.00 | 163,356,894.27 | 4,166,530,394.27 | 2,592,112,589.21 | 62.21 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| to ya fungiwa | 1,496,641,000.00 | 60,431,197.14 | 1,557,072,197.14 | 574,076,814.31 | 36.86 |
| ku ya mizi ineyo | 742,884,000.00 | 0 | 742,884,000.00 | 424,376,142.66 | 57.12 |
| ku ya ahara | 16,864,799,000.00 | 0 | 16,864,799,000.00 | 11,696,263,500.00 | 69.35 |
| ku ya di ya ndeleo | 14,251,509,522.51 | | 14,251,509,522.51 | 6,139,945,653.33 | 43.08 |
| **LA KUU** | **37,359,007,022.51** | **223,788,091.41** | **37,582,795,113.92** | **21,426,774,699.51** | **57.01** |

Wajumbe walipokea taarifa nakuijadili kama ifuatavyo,

**Kuhusu fedha za miradi ya maendeleo.**

Mheshimiwa Ngwinde alieleza kuwa fedha za miradi ya maendeleo ianishwe kwa kuwa fedha za 10% ya vijana,wanawake na watu wenye ulemavu ipo kwenye fedha hizi za miradi ya maendeleo,fedha hizi ziainishwe kama zilivyoainishwa fedha za miradi ya uviko 19.Aidha alieleza kuwa ripoti ya ukaguzi inaonyesha kuwa Halmashauri inadaiwa fedha za miradi ya maendeleo,hivyo tuletewe mchanganuo wa fedha za miradi ya maendeleo.

Kaimu mwekahazina wa wilaya alitoa ufafanuzi kuwa si kila fedha zinazoingia zinagawanywa katika miradi ya maendeleo,fedha zinatumika kulingana na vipaumbele vya Halmashauri kwa muda huo,ikitokea tumekusanya fedha za kutosha ndio tunapeleka moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti alieleza kuwa hata kama fedha za miradi ya maendeleo zimetumika katika matumizi mengine ya Halmashauri,mchanganuo uletwe unaoonyesha fedha mlizokopa ili tujue fedha zinazotakiwa kwenye miradi ni kiasi gani mpaka sasa.

Wajumbe waliazimia kuwa kikao kijacho iletwe taarifa ya mchanganuo wa fedha za miradi ya maendeo ilitengwa kwa mwaka huu wa fedha,fedha zilizopekwa kwenye miradi,miradi iliyopelekewa hizo fedha na fedha zilizobaki kama zilikopwa ni kiasi gani.

Mheshimiwa Ngwinde alieleza Kuhusu fedha zinazoletwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo,kwamba fedha zinaletwa lakini zinachelewa kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo, hii inayonyesha kuwa vifungu vya kuhamishiwa fedha haziandaliwi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti alisisitiza kuwa fedha zilizoletwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo yafanyiwe michakato ya haraka ili fedha hizo ziende kwenye miradi ya maendeleo na tupate mrejesho wa suala hilo.

**Kuhusu ushuru wa kuegesha malori na ushuru wa stendi.**

Mheshimiwa Ngwinde alitaka kufahamu kuhusu ushuru wa kuegesha magari stendi.

Kaimu mwakahazina alitoa ufafanuzi kuwa ushuru wa kuegesha magari kama vile, ushuru wa malori yanayopaki Nangurukuru na Somanga,na ushuru wa stendi ni ushuru wa magari ya abiria. Aidha alifafanua Zaidi kuwa bei za kutoza ushuru kwa magari kama probox ni Tsh.500/=kwa siku,Coster 1000/=kwa siku na basi ni 2000/=kwa siku.
Mjumbe alieleza kuwa bado ukusanyaji wa ushuru wa maegesho ya magari na magari ya abiria haujakusanywa ipasavyo.

Afisa mapato alieleza kuwa ni kweli kuna changamoto kwenye eneo la ukusanyaji wa ushuru wa magari ya abiria, nah ii hutokana na muda mwingine mkusanyaji wetu kutokuwepo stendi wakati magari yanaondoka,pia kutokuwepo kwa kuzuizi cha masakasa. Aidha tutaanzisha kizuizi cha masakasa na tutamsihi mkusanyaji wa ushuru wa stendi awepo ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Halmashauri.

Wajumbe waliazimia kuwa watafuatilia vyanzo vyote vya mapato ili kubaini tatizo la kushuka kwa mapato hasa mapato yanayotokana na stendi.

**Kuhusu ukodishwa mali za Halmashauri.**
Mheshimiwa mwenyekiti alihoji mali za Halmshauri zinazokodishwa ni zipi.
Afisa mapato alitoa ufafanuzi kuwa mali zinazokodishwa na Halmashauri ni vibanda vya hapa masoko na Kivinje,pia kisiwa cha Fanjove ni sehemu ya mali ya Halmashauri inayokodishwa.

Mheshimiwa mwenyekiti alihoji makusanyo ya Tsh.8,000,000/= toka kisiwa cha Fanjove ni kwa muda gani.
Afisa mapato alitoa ufafanuzi kuwa fedha hizo zimekusanywa kwa mwaka mmoja.

Wajumbe waliazimia kuwa iletwe taarifa ya utambuzi wa kampuni ya Fanjove huko kisiwani,kampuni hiyo ipo kwa muda gani na inajishughulisha na kazi gani.

**Kuhusu makusanyo ya ufuta kwa mwaka wa fedha 2021/2022**
Wajumbe waliazimia kuwa iwasilishwe taarifa za minada ya ufuta iliyofanyika kuazia mwezi mei hadi Juni,2021 na Julai hadi Agosti,2022.

## 2022. MAPOKEZI YA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SEKTA YA AFYA

Halmashauri imepokea fedha jumla ya kiasi cha kiasi cha shilingi 670,714,400 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Sekta ya afya ya mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo:

| Kiasi cha Fedha kilichopokelewa | Chanzo cha fedha | Jina la mradi | Aina ya majengo yatakayojengwa/kukarabatiwa | Changamoto iliyopo | Utatuzi wa changamoto |
|---|---|---|---|---|---|
| [illegible] | Serikali Kuu (Fedha za | Kuendeleza ujenzi wa | Jengo la Uzazi lililounganishwa | Fedha zilizotolewa na | Inahitajika itengenezwe |

| Kiasi cha Fedha kilichopokelewa | Chanzo cha fedha | Jina la mradi | Aina ya majengo yatakayojengwa/kukarabatiwa | Changamoto iliyopo | Utatuzi wa changamoto |
|---|---|---|---|---|---|
| | Tozo) | kituo cha afya kata ya Mandawa kilichopo katika kijiji cha Hotelitatu | ná jengo la Upasuaji<br><br>ii)Jengo la kufulia nguo<br><br>iii)Korido za kuunganisha majengo | Serikali ni kidogo ikilinganishwa na aina ya majengo yanayojengwa. | BOQ itakayoonyesha maksio halisi ya kujenga majengo haya 3 ili kubaini upungufu uliopo na kutafuta njia ya kutatua. |
| 90,000,000 | Serikali Kuu.<br><br>(Fedha za IMF) | Ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika kituo cha afya Hotelitatu | -Ujenzi wa nyumba ya watumishi 3:1 katika kituo cha afya hotelitatu. | Maksio ya kihandisi yanaonyesha kuwa gharama ya kujenga nyumba hii ya watumishi ya 3:1 ni sh.127,504,623.84 lakini fedha zilizoletwa ni sh. 90,000,000 Hivyo kuna upungufu wa fedha shilingi 37,504,623.84 | Kununua vifaa vya ujenzi kwa bei ya soko, na<br><br>Kuangalia uwezekano wa kupata fedha kutoka vyanzo vingine ili kuziba upungufu uliopo ili kuwezesha mradi kukamilika. |
| 300,000,000 | Serikali Kuu.<br><br>(Fedha za IMF) | Ujenzi wa jengo la dharura katika hospitali ya wilaya Kinyonga | -Ujenzi wa Jengo la dharura<br><br>(Emergency Health Department - EMD) | Maksio ya kihandisi yanaonyesha kuwa gharama ya kujenga jengo hili la dharura ni sh. 399,112,221.84 lakini fedha zilizoletwa ni sh. 300,000,000/=<br><br>Hivyo kuna upungufu wa fedha sh. 99,112,221.84 | Kununua vifaa vya ujenzi kwa bei ya soko, na<br><br>Kuangalia uwezekano wa kupata fedha kutoka vyanzo vingine ili kuziba upungufu uliopo na kuwezesha mradi kukamilika. |
| 25,000,000 | Serikali kuu.<br><br>(Fedha za UVIKO 19) | Kukarabati jengo la kulaza wagonjwa wa Uviko 19 | Kukarabati jengo la kulaza wagonjwa wa Uviko 19 | Hatuna jengo Maalum la kulaza wagonjwa wa UVIKO 19 ila tunazo wodi za | Inahitajika itengenezwe Maksio ya ukarabati wa jengo la Uviko 19 ili kufahamu gharama |

| Kiasi cha Fedha kilichopokelewa | Chanzo cha fedha | Jina la mradi | Aina ya majengo yatakayojengwa/kukarabatiwa | Changamoto iliyopo | Utatuzi wa changamoto |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| . | | katika hospitali ya wilaya Kinyonga | | kawaida za kulaza wagonjwa. Wodi mojawapo itakarabatiwa kwa ajili ya kusudi hili. | halisi ya ukarabati huu kulingana na hali ya jengo |
| 5,214,400 | Fedha za uviko 19 | Malipo ya mtumishi wa mkataba toka Tamisemi | Stahiki za mtumishi | | |
| 670,714,400 | | | | | |

Mganga mkuu wa wilaya alitoa ufafanuzi Zaidi kuhusu mapokezi ya fedha hizo kuwa zimeletwa ili kujenga majengo matatu ambazo Jengo la Uzazi lililounganishwa na jengo la Upasuaji,Jengo la kufulia nguo na Korido za kuunganisha majengo kwa Tsh.250,000,000/=na zimeletwa na ramani ya majengo hayo, lakini fedha hizo hazitatosha kujenga majengo hayo.

Wajumbe walijadili suala hilo kwa kina nakukubaliana kuwa majengo yajengwe kulingana na fedha zilizoletwa bila kuathiri ramani iliyoletwa,aidha taarifa itolewe TAMISEMI baada ya fedha kuisha.

Mganga mkuu wa wilaya alipokea ushauri huo nakueleza kuwa atalifanyia kazi.

**22.TAARIFA YA ZIARA YA WENYEVITI WA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI NA WATAALAM KWENDA KUJIFUNZA NA KUTEMBELEA MAGHALA YANAYOHIFADHI MAZAO YA WAKULIMA NANGURUKURU,HALMASHAURI ZA MTAMA,RUANGWA NA NACHINGWEA.**

Mwandishi wa mikutano aliwasilisha taarifa ya ziara ya wenyeviti wa kamati za kudumu za Halmashauri na wataalam,ziara hiyo ilikuwa na lengo la kupata elimu juu ya uendeshaji wa maghala na namna ambavyo maghala yanaongeza mapato kwenye Halmashauri. Aidha timu hiyo ya wenyeviti na wataalam wakatoa mapendekezo yao na kujadiliwa na wajumbe wa kamati ya fedha,uongozi na mipango, na kamati kutoa mapendekezo yafuatayo juu ya uendeshaji wa ghala la Nangurukuru kwa mwaka huu.

i. Wajumbe walikubaliana kwa pamoja kutokana na elimu ya uendeshaji tulioipata kutoka kwa wenzetu kwa mwaka utaokuja tutaanzisha mchakato wa kuunda kampuni ambayo itakua ndio msimamizi wa ghala hilo

ii. Taarifa za kutangazwa Mzabuni itangazwe mapema sana na wazabuni watakaoomba washindanishwe kwa kuzingatia sharti la bei ya Kilo 1 isiwe chini ya Tsh.10 na mzabuni atakaeomba awe na mizani zaidi ya moja na za kisasa ili kupunguza changamoto kutoka kwa wateja

## 1/2022.MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

### 31.1.KUHUSU UEZEKAJI WA SOKO LA SAMAKI KIVINJE.

Mheshimiwa Arobaini alitaka kufahamu uezekaji wa jengo la soko la samaki Kivinje utakamilika lini.

Kaimu Mhandisi wa wilaya alieleza kuwa tathmini ya kukamilisha ujenzi wa soko la samaki Kivinje ulishakamilika na maombi yakukamilisha ujenzi wa soko ilishapelekwa kwa Mkurugenzi mtendaji wa wilaya kwa ajili ya utekelezaji zaidi.

Mheshimiwa Arobaini alihoji gharama za ukamilishaji wa ujenzi wa soko la samaki Kivinje ni kiasi gani.

Kaimu Mhandisi wa Wilaya alitoa ufafanuzi kuwa hana kumbukumbu sahihi kwa muda ule kwakuwa umepita muda tangu maombi hayo yaandaliwe.

Kaimu Afisa Mipango wilaya alieleza kuwa hoja hii ni ya muda mrefu,tuliomba vifungu lakini kuna baadhi ya vifungu havikurudi, aidha Halmashauri itakamilisha ujenzi wa soko japo mradi huu haukuwa kwenye bajeti ya mwaka huu.

Wajumbe waliazimia kuwa kikao kijacho tupate taarifa ya hatua iliyofikiwa katika ukamilishaji wa ujenzi wa soko la samaki Kivinje.

### 31.2. KUHUSU UJENZI WA STENDI YA MABASI NANGURUKURU.

Wajumbe walitaka kufahamu maendeleo ya mradi wa stendi wa mabasi Nangurukuru umefikia hatua gani.

Mhandisi wa ujenzi Wilaya alitoa ufafanuzi kuwa kwasasa tunaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa choo,pia kuna fedha tumeomba kwa ajili uwekaji wa vifusi na kuweka urembo sehemu ya kukaa abiria.

Wajumbe waliazimia kuwa kikao kijacho tupate taarifa katika mwaka huu wa fedha mradi wa stendi ya Nagurukuruum umetengewa bajeti ya fedha kiasi gani.

### 31.3.TAARIFA YA MAPOKEZI YA GARI.

Mganga Mkuu wa Wilaya alitoa taarifa ya mapokezi ya gari toka mradi wa BORESHA AFYA iliyofanya kazi kwa karibu na Vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya,aidha kwasasa muda wao wa kufanya kazi katika Halmashauri ya Kilwa umeisha,hivyo wameiachia Halmashauri gari kwa ajili ya matumizi ya Halmashauri.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo,aidha walimpongeza Mganga Mkuu wa Wilaya kwa kuisaidia Halmashauri kupata gari.

### 31.4.KUHUSU TAARIFA YA UJENZI WA SHULE SHIKIZI NANGOLOMBE-KANDAWALE.

Mheshimiwa Kimbungu alieleza kuwa shule shikizi ya Nangolombe ina jumla ya madarasa matatu,na darasa moja linajengwa tena na wananchi kwa nguvu zao wenyewe,alihoji ni lini shule shikizi ya Nangolombe itapata usajili wa kudumu ili

wanafunzi wasome katika shule ili kupunguza wanafunzi kutembea umbali mrefu kutafuta elimu.

Kaimu Afisa mipango alitoa ufafanuzi kuwa changamoto iliyopo ni fedha,tuliomba fedha toka TASAF shilingi 80,000,000/=kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa yaliyobaki lakini bado hizo fedha hazijapatikana.

Wajumbe waliazimia kuwa tupate taarifa za kina kuhusu shule hiyo,pia tupate taarifa ya usajili wa shule shikizi ya Nangolombe Kata ya Kandawale.

**32/2022.KUFUNGA KIKAO.**

Katibu aliwashukuru wajumbe, pamoja na Wataalamu kwa majadiliano ambayo yataleta ustawi katika Halmashauri yetu, Alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa uvumilivu wao,aidha aliwasihi tuwe kitu kimoja ili tuweze kuiletea maendeleo Halmashauri yetu ya Kilwa,baada ya hapo alifunga Kikao mnamo saa 11:55 Jioni.

SAINI YA MWENYEKITI..................... SAINI YA KATIBU.....................

TAREHE..26/5/2022.........................